Halifax
Regional Centre for Education

| Msaada kwa wanafunzi na wafanyakazi katika shule za HRCE | |
|---|---|
| | |
| **English** | Kiswahili |
| **HRCE Parent Navigator (located at HRCE central office)**<br><br>The role of the Parent Navigator is to help parents and guardians of students find and access services available in education, justice, health, community services and more.<br><br>They can help you find the support that you or your child may need to achieve success, inside and outside of school. They will help guide and connect you with the most appropriate services and resources. Reach out!<br>Contact Information:<br>902-464-2000 extension 4361<br><br>**SchoolsPlus (located in schools)**<br><br>SchoolsPlus is a confidential, free service available in every school in Nova Scotia. Our goal is to build positive relationships between families, schools, and communities. If you have many services connected with your family, our facilitators can help bring everyone together and make a supportive plan for you. We also have Community Outreach Workers who can connect you to resources in your community. You can self-refer to SchoolsPlus for 12 months a year. Contact the SchoolsPlus Facilitator at your school or email schoolsplus@hrce.ca | **Programu ya mzazi kuangalia vitu mbalimbali kwenye HRCE (iliyowekwa katika ofisi kuu ya HRCE)**<br><br>**Programu ya mzazi kuangalia vitu mbalimbali** ni kusaidia wazazi na walezi wa wanafunzi kufikia huduma zinazopatikana katika elimu, haki, afya, huduma za jamii na zaidi.<br><br>Inaweza kukusaidia kupata msaada ambao wewe au mtoto wako mnaweza kuhitaji ili kufikia mafanikio, ndani na nje ya shule. itakusaidia kukuongoza na kukuunganisha na huduma na rasilimali zinazokufaa zaidi. Ulizia!<br>Kwa Mawasiliano piga:<br>902-464-2000 ungani 4361<br><br>**SchoolsPlus (zilizo ndani ya shule)**<br><br>SchoolsPlus ni huduma ya siri, na bure inayopatikana katika kila shule humu Nova Scotia. Lengo letu ni kujenga uhusiano mzuri kati ya familia, shule, na jamii. Ikiwa una huduma nyingi zilizounganishwa na familia yako, wasaidizi wetu wanaweza kusaidia kumleta kila mtu pamoja na kukutengenezea mpango unao kusaidia wewe. Pia tuna Wafanyakazi wa Jamii ambao wanaweza kukuunganisha na rasilimali katika jamii yako. Unaweza kuja kwenye SchoolsPlus kwa miezi 12 kwa mwaka. Wasiliana na Mwezeshaji wa Shule katika shule yako au tumia barua pepe schoolsplus@hrce.ca |

**YMCA School Settlement Staff**

The YMCA works in partnership with over 40+ schools in the greater Halifax area to assist Permanent Resident immigrant children, youth, and their families. Our friendly, welcoming YMCA School Settlement Support Staff work on-site at elementary, junior and senior high schools to provide practical assistance to immigrant children, youth, and families.

Our YMCA staff provide individualized support at all School Settlement Program locations to ensure that students and families feel confident, comfortable and most of all, connected to your community, including:

- Orientation to your new school and community
- Liaising between home and school
- Referrals to settlement, language, and employment services
- Becoming connected with local services suited to your needs
- After school programs and various recreational activities
- Help with your schoolwork through YMCA academic counselling, Homework Clubs, and peer tutoring
- Assistance with language translation and interpretation
- Making new friends and engaging with others at the YMCA multicultural clubs and events

**African Nova Scotian Student Support Worker Program**

The African Nova Scotia Student Support Worker Program provides in-school support for African Nova Scotian students, and students of African ancestry, to ensure improved achievement through a positive school experience. Student Support Workers

**Wafanyakazi wa YMCA Shuleni Kwa ajili ya Wahamiaji**

YMCA inafanya kazi kwa kushirikiana na shule zaidi ya 40 katika eneo kubwa la Halifax kusaidia watoto wa wahamiaji wa kudumu, vijana, na familia zao. Wafanyakazi wetu wema wa YMCA Shuleni wanaosaidia wahamiaji, hufanya kazi katika shule za msingi, na sekondari ili kutoa msaada wa vitendo kwa watoto wahamiaji, vijana, na familia.

Wafanyakazi wetu wa YMCA hutoa msaada unaomlenga mtu binafsi katika maeneo yote ya Programu kwa wahamiaji Shuleni ili kuhakikisha kuwa wanafunzi na familia wanasikia ujasiri, starehe na zaidi ya yote, kuunganishwa na jamii yako, ikiwa ni pamoja na:

- Maelekezo kwa shule yako mpya na jamii
- Uhusiano kati ya nyumbani na shuleni
- Marejeleo ya makazi, lugha, na huduma za ajira
- Kuunganishwa na huduma za sehemu unapoishi zinazofaa kwa mahitaji yako
- Mipango ya baada ya shule na shughuli mbalimbali za burudani
- Msaada na kazi za shule kupitia ushauri wa kimasomo wa YMCA, Vilabu vya Kazi za shule nyumbani, na kufundishwa na wanarika
- Msaada kwa tafsiri na ukalimani wa lugha
- Kupata marafiki wapya na kushirikiana na wengine katika klabu na matukio ya kitamaduni ya YMCA

**Programu ya Mfanyakazi wa Kusaidia Mwanafunzi mwenye asili ya Afrika wa Nova Scotia**

Programu ya Wafanyakazi wa Msaada kwa Wanafunzi wenye asili ya Afrika wa Nova Scotia hutoa msaada ndani ya shule kwa

provide supports that align with the Inclusive Education Policy. School-based programming provides valuable opportunities for students of African ancestry to build supportive relationships, cultural awareness and increased self-esteem towards learning, academic achievement, and student well-being. This support is provided through four pillars of their role: Home and School Liaison, Classroom Support, Cultural Enrichment Programs and Student Advocacy. If you have questions about the African Nova Scotian Student Support Worker Program contact your school principal.

**Pre-primary Education**

The Pre-primary Program is a universal play based program for four-year-olds, with no cost to families, in the province. The program is offered in the school setting which helps children to transition into Primary the following year. Your child must be turning four years of age by December 31st to be eligible to register for Pre-Primary in the current school year.

Some families may also be eligible for busing.

To find a program near you, to register, or to learn more about the program, please contact 902-464-2000 or visit our Pre-Primary website.

**English as an Additional Language (EAL)**

The EAL Teacher is responsible for providing specialized English as an Additional Language instruction to students whose English proficiency ranges from beginner to advanced levels in listening, speaking, reading and writing. The EAL teacher works with administrators and classroom/subject teachers to plan appropriate programming and service delivery alternatives for EAL students.

wanafunzi WaNova Scotia wenye asili ya Afrika, na wanafunzi ambao wazazi wao wanatoka Afrika, ili kuhakikisha mafanikio chanya shuleni. Wafanyakazi wa Msaada wa Wanafunzi hutoa msaada unaoendana na Sera ya Elimu Jumuishi. Programu ya msingi ya shule hutoa fursa muhimu kwa wanafunzi wenye asili ya Afrika kujenga uhusiano wa kuungana mkono, ufahamu wa utamaduni na kuongeza kujiamini kuhusu kujifunza, mafanikio ya kimasomo, na ustawi wa wanafunzi. Msaada huu hutolewa kupitia nguzo nne za jukumu lao: kuunganisha maswala ya nyumbani na shuleni, Msaada Darasani, Programu za Kuboresha Utamaduni na Utetezi wa Wanafunzi. Ikiwa una maswali kuhusu Programu ya Wafanyakazi wa Msaada kwa Wanafunzi wa Nova Scotia wenye asili ya Afrika wasiliana na mkuu wako wa shule.

**Elimu ya Awali**

Programu ya kabla ya shule ya msingi ni mpango wa kucheza kwa watoto wa miaka minne, bila gharama kwa familia, katika provinsi. Mpango huo hutolewa katika mazingira ya shule ambayo husaidia watoto kuwa tayari ili kuingia shule ya Msingi mwaka unaofuata. Mtoto wako lazima awe na umri wa miaka minne ifikapo Desemba 31 ili astahili kuandikishwa kwa ajili ya shule ya awali katika mwaka wa sasa wa shule.

Baadhi ya familia zinaweza pia kuwa na haki ya huduma za basi.

Ili kupata programu karibu na wewe, kujiandikisha, au kujifunza zaidi kuhusu programu, tafadhali wasiliana na 902-464-2000 au tembelea tovuti yetu ya Pre-Primary.

**Kiingereza kama lugha ya ziada (EAL)**

Mwalimu wa EAL ana jukumu la kufundisha Kiingereza maalum kama mafunzo ya ziada ya lugha kwa wanafunzi ambao ustadi wao wa Kiingereza uko chini hadi ule wa viwango vya juu katika kuelewa, kuzungumza, kusoma na kuandika. Mwalimu wa EAL anafanya kazi na wasimamizi na walimu wa

| | |
|---|---|
| | darasa / walimu wa masomo ili kupanga programu zinazofaa na njia mbadala za utoaji wa huduma kwa wanafunzi wa EAL. |
| **Assistive Technology**<br><br>All individuals use strategies and devices to assist them in performing tasks more efficiently and effectively on various occasions. Students with diverse learning needs may need a range of assistive technologies in order to participate more fully in daily activities and to meet learning outcomes. | **Teknolojia saidizi**<br><br>Watu wote hutumia mikakati na vifaa kuwasaidia katika kutekeleza majukumu kwa ufanisi zaidi na kwa ufanisi katika maswala mbalimbali. Wanafunzi wenye mahitaji mbalimbali ya kujifunza wanaweza kuhitaji teknolojia mbalimbali za kusaidia ili kushiriki kikamilifu katika shughuli za kila siku na kufikia matokeo mazuri ya kujifunza. |
| **Autism Specialists**<br><br>The Autism Specialists work collaboratively with school-based staff and other professionals to support programming for students diagnosed with Autism Spectrum Disorder (ASD) to maximize student learning experiences. Autism Specialists support Student Planning Teams in the areas of curricular assessment, programming, teaching strategies and transitions for students with Autism Spectrum Disorders. Early transition support is provided to all students with an ASD diagnosis who enter HRCE schools during their primary year. | **Wataalamu wa Usonji**<br><br>Wataalamu wa Usonji hufanya kazi kwa kushirikiana na wafanyakazi wa shule na wataalamu wengine kusaidia kupanga programu kwa wanafunzi waliogunduliwa na ugonjwa wa Usonji (ASD) ili kuongeza ubora wa jinsi ya wanafunzi kujifunza. Wataalamu wa Usonji wanasaidia Timu za Mipango ya kutathimini mitaala, programu na mikakati ya kufundisha na mpito kwa wanafunzi walio na Matatizo ya Usonji. Msaada wa mpito wa mapema hutolewa kwa wanafunzi wote waliopatikana na Usonji ambao huingia shule za HRCE wakati wa mwaka wao wa shule ya msingi. |
| **School Counsellors**<br><br>School Counsellors support student well-being and achievement by developing and providing primarily short term counselling services to individuals, small groups, and classes of students on a variety of mental health and well-being topics. School Counsellors regularly partner with school based staff, families and community based service providers in supporting student well-being. Each school has access to a school counsellor. Referral for this service must be made through the school. | **Washauri wa Shuleni**<br><br>Washauri wa Shuleni wanasaidia ustawi wa wanafunzi na mafanikio kwa kuendeleza na kutoa huduma za ushauri wa muda mfupi kwa watu binafsi, vikundi vidogo, na madarasa ya wanafunzi juu ya mada mbalimbali za afya ya akili na ustawi. Washauri wa Shule mara kwa mara hushirikiana na wafanyakazi walioko shuleni, familia na watoa huduma wa jamii katika kusaidia ustawi wa mwanafunzi. Kila shule ina uwezo wa kupata mshauri wa shuleni. Maombi ya huduma hii lazima yafanywe kupitia shule. |
| **Resource and Learning Centre Teachers** | |

| | |
|---|---|
| Programming and services provided by Resource and Learning Centre teachers are intended to assist students in achieving the learning outcomes of the Public School Program (PSP) curriculum or, in the case of students with an IPP, their individualized outcomes. Collaboration is critical to ensuring the essential relationship between support and outcomes. This is facilitated through the participation of both the learning support teachers and classroom teachers in the program planning process.<br><br>**School Psychologist**<br><br>The School Psychologist supports the school team by providing knowledge and skills in the areas of assessment, counselling and consultation in relation to curriculum and social outcomes for students. Each school has access to this service on an itinerant basis. Referral for this service must be made through the Teaching Support Team.<br><br>**Behaviour Specialists**<br><br>There are students in our schools who exhibit significant behaviour difficulties and are in need of specialized assessment and intervention. Initiation of service is with the Teaching Support Team, who may decide to refer to the school psychologist. If the Teaching Support Team and school psychologist determine that more extensive intervention is required, a referral may be made to the Behaviour Specialist.<br><br>**Speech-Language**<br><br>The Speech-Language Pathologist supports the school team by providing knowledge and skills in the area of communication development, and assisting students with speech and language disorders in meeting | **Walimu wa Kituo cha Usaidizi wa Kujifunza**<br>Programu na huduma zinazotolewa na walimu wa Kituo cha Usaidizi wa Kujifunza zinakusudiwa kusaidia wanafunzi katika kufikia matokeo ya kujifunza ya mtaala wa Programu ya Shule ya Umma (PSP) au, kwa upande wa wanafunzi walio na IPP, matokeo yao ya kibinafsi. Ushirikiano ni muhimu katika kuhakikisha uhusiano muhimu kati ya msaada na matokeo. Hii inawezeshwa kupitia ushiriki wa walimu wa msaada wa kujifunza na walimu wa darasa katika mchakato wa kupanga programu.<br><br>**Mwanasaikolojia wa Shuleni**<br><br>Mwanasaikolojia wa Shuleni anasaidia timu ya shule kwa kutoa maarifa na ujuzi katika maeneo ya tathmini, ushauri na ushikiano kuhusiana na mtaala na matokeo ya kijamii kwa wanafunzi. Kila shule ina upatikanaji wa huduma hii kwa mpangilio wa wao kumwitwa shuleni anapohitajika. Rufaa ya huduma hii lazima ifanywe kupitia Timu ya Usaidizi wa Kufundisha.<br><br>**Wataalamu wa Tabia**<br><br>Kuna wanafunzi katika shule zetu ambao huonyesha matatizo makubwa ya tabia na wanahitaji tathmini maalum ili kuingilia kati. Kuanzisha huduma kunatokana na Timu ya Msaada wa Kufundisha, ambao wanaweza kuamua kumpeleka kwa mwanasaikolojia wa shuleni. Ikiwa Timu ya Msaada wa Kufundisha na mwanasaikolojia wa shule wataona kuwa msaada mkubwa zaidi unahitajika, rufaa inaweza kufanywa kwa Mtaalam wa Tabia.<br><br>**Kuongea-Lugha**<br><br>Mtaalamu wa kuongea-Lugha anasaidia timu ya shule kwa kutoa maarifa na ujuzi |

<table>
<tr>
<td>
curriculum and social outcomes. Each school has access to this service on an itinerant basis. Referral for this service must be made through the Teaching Support Team.<br>
Social Workers<br><br>
As a member of the school team, the Social Worker collaborates with school staff in responding to the needs of students who may be experiencing personal, family, or social difficulties.<br><br>
School Social Workers can help students, families and/or schools when the following issues arise:<br>
<ul>
<li>aggression and anger</li>
<li>alcohol and/or drug use/abuse</li>
<li>attendance problems</li>
<li>behavioral problems</li>
<li>child abuse and neglect</li>
<li>classroom problems</li>
<li>communication difficulties</li>
<li>death or grief</li>
<li>parenting questions</li>
<li>poor peer relationships and social skills</li>
<li>remarriage separation/divorce</li>
<li>self-esteem</li>
<li>sexuality questions</li>
<li>stress</li>
<li>suicidal thoughts</li>
<li>teenage pregnancy</li>
</ul>
</td>
<td>
katika eneo la maendeleo ya mawasiliano, na kusaidia wanafunzi wenye matatizo ya kuzungumza na lugha katika kufikia mtaala na<br>
matokeo mazuri kitabia. Kila shule inaweza kupata huduma hii kwa njia ya kumwita mtaalam. Rufaa ya huduma hii lazima ifanywe kupitia Timu ya Usaidizi wa Kufundisha.<br><br>
Wafanyakazi wa Usitawi wa jamii<br><br>
Kama mmoja wa timu ya shule, Mfanyakazi wa Ustawi wa Jamii hushirikiana na wafanyakazi wa shule katika kukabiliana na mahitaji ya wanafunzi ambao wanaweza kuwa na shida za kibinafsi, familia, au kijamii.<br>
Wafanyakazi wa Ustawi wa Jamii wa Shule wanaweza kusaidia wanafunzi, familia na / au shule wakati masuala yafuatayo yanatokea:<br>
<ul>
<li>Ugomvi na hasira</li>
<li>Pombe na/au matumizi ya madawa ya kulevya</li>
<li>Matatizo ya mahudhurio</li>
<li>Matatizo ya tabia</li>
<li>Unyanyasaji wa watoto na kutelekezwa</li>
<li>Matatizo ya darasani</li>
<li>Matatizo ya mawasiliano</li>
<li>Kifo au huzuni</li>
<li>Maswali ya malezi</li>
<li>mahusiano duni na wanarika na kukosa ujuzi wa mahusiano mazuri</li>
<li>Ndoa za pili/ Kutengana na kuachana</li>
<li>Kutokujiamini</li>
<li>Maswali ya ujinsia</li>
<li>Msongo wa mawazo</li>
<li>Mawazo ya kujiua</li>
<li>mimba ya ujanani</li>
</ul>
</td>
</tr>
</table>